BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA NANE

Kikao cha Kumi – Tarehe 20 Septemba, 2022.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kwa mwaka 2021/2022.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kuhusu Ripoti ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kwa mwaka 2021/2022.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

79. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

    Ndani ya Muungano wetu wa Tanzania ziko Wizara maalum za Muungano ambapo wafanyakazi wake hutokea pande zote mbili Washirika wa Muungano, yaani Tanzania bara na Zanzibar. Inafahamika wazi kwamba kupitia ajira hizo za Muungano,

Zanzibar hupatiwa mgao wake wa asilimia 21, ingawaje utekelezaji wa mgao huo unaonekana kusuasua kwa muda sasa.

(a) Je, kwa kiasi gani utekelezaji wa mgao huo unafanyika kama ulivyopangwa.

(b) Kama utekelezaji huo unafanyika, Je, ni nafasi ngapi za ajira za Muungano zilitoka kwa mwaka 2021 na upi ulikuwa mgao wa kila mshirika wa Muungano, taasisi kwa taasisi za washirika hao.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

115. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Ni jambo la kuipongeza Serikali kwa kuwapandishia watumishi wake viwango vya mishahara kwa kiwango kinachoridhisha. Hata hivyo, kuna wafanyakazi ambao malipo yao yanapitia kwa wafanyakazi wengine wa Serikali (kwa mfano watumishi, wasaidizi na madereva wa Waheshimiwa Wawakilishi), ambao malipo yao hayakuongezeka hata kidogo ukilinganisha na watumishi kama wao ambao wameongezewa mishahara kwa hadi au zaidi ya asilimia 23.3.

(a) Je, kuna sababu zipi zilizopelekea hali hiyo.

(b) Je, ni lini Serikali itawafanyia marekebisho ya malipo mapya wafanyakazi wanaopata malipo yao kupitia Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

138. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uwekezaji:

Kwa kuwa kumekuwa na taarifa nyinyi zenye kutofautiana juu ya takwimu za vijana wasiokuwa na ajira Zanzibar, na kwa kuwa kitendo cha kuwa taarifa sahihi juu ya jambo husika kinaisaidia Serikali kupanga vyema shughuli zake.

(a) Je, ni zipi takwimu sahihi za vijana wasiokuwa na ajira nchini.

(b) Je, kiwango *(rate)* cha ongezeko la vijana wasiokuwa na

ajira ikoje.

<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>

140. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Tunaipongeza Serikali kwa kuendeleza ujenzi wa masoko hapa nchini.

(a) Je, ujenzi wa Soko la Machomane unatarajiwa kugharimu kiasi gani mpaka kukamilika kwake.

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kimeshatumika katika ujenzi huo hadi hivi sasa.

<u>Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>

114. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Ilishazoeleka kwamba mmoja katika viongozi waandamizi wa Wizara dhamana na Fedha (kwa mfano Naibu Katibu Mkuu) anakuwa mmoja katika wajumbe wa Bodi ya Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), ili kuweza kuitetea Benki na kuona kwa karibu changamoto za PBZ katika soko la ushindani. Hata hivyo, kwa sasa Naibu Katibu Mkuu sio mjumbe wa Bodi ya PBZ.

Je, ni kwa nini imekuwa hivyo na nani mtetezi wa PBZ wa moja kwa moja kutoka Wizara dhamana na Fedha.

<u>Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:</u>

73. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Uhifadhi wa taarifa za Serikali kieletroniki ni njia muhimu sana ambapo nchi nyingi ulimwenguni zinaitumia njia hii kuhifadhia taarifa za Serikali zao. Hata hivyo, hapa kwetu Zanzibar Sehemu yetu Kuu ya Kuhifadhia taarifa za Serikali Kieletroniki (Data Centre) ni ndogo sana ukilinganisha na ukuaji wa taarifa za kila siku za Serikali:

(a) Je, Serikali haioni haja ya kukitanua kituo chake mahsusi na kinacho jitegemea cha 'Data Centre'.

(b) Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi mahsusi wa kituo chake hicho cha 'Data Centre'.

<u>Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:</u>

87. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kwa kipindi kirefu sasa kumekuwa na malalamiko ya watumiaji wa ving'amuzi vya Kampuni ya Zanzibar Cable TV (ZCTV) kwamba wanatakiwa kulipia ving'amuzi vipya mara kwa mara, hali ambayo inaleta kero kubwa kwa watumiaji wa ving'amuzi hivyo.

(a) Kwa kuwa Wizara yako ndio yenye dhamana kwa vyombo vyote vya habari hapa Zanzibar, Je, ni hatua gani ilizozichukua kuondoa kero hiyo.

(b) Je, ni sababu gani hasa zilizoipelekea Kampuni hiyo kubadilisha ving'amuzi vyao na kuwalipisha watumiaji malipo mapya mara kwa mara.

<u>Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:</u>

159. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Tunaishukuru Serikali kwa kuhimiza na kuwafanyia nafuu wakulima, hali inayoinua kilimo na kuongeza kipato kwa wakulima wetu.

(a) Je, kuna matrekta mangapi na ya aina gani yanayotumika kwa kilimo nchini mwetu.

(b) Je, ni mangapi kati ya matrekta hayo mazima na mangapi ni mabovu.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

123. MHESHIMIWA MWANAASHA KHAMIS JUMA (Jimbo la Dimani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa Skuli ya Kisauni ni skuli ya muda mrefu na sasa hivi haina eneo la kutosha la kuongeza mabanda ya madarasa ili kupunguza mrundikano wa wanafunzi. Na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu aliyepita, aliwahi kufanya ziara na kuona hali halisi ya ufinyu wa eneo na mrundikano wa wanafunzi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kulinunua eneo jengine liliopo mkabala na skuli hiyo kwa ajili ya kuongeza mabanda ya madarasa na kuondosha msongamano wa wanafunzi uliopo sasa.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

Ripoti ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kwa mwaka 2021/2022.

Zanzibar, (Raya Issa Msellem)
20 Septemba, 2022. **KATIBU WA BARAZA.**